**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari Bukoba,**

**S.L.P. 52,**

**BUKOBA**

**Tarehe 12/6/2023**

***Namba za Simu***

***Mkuu wa Shule 0754 076 905***

***Makamu Mkuu wa Shule 0765 051 660***

***Matron/Patron 0768 822 791***

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………......................................................................….**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUKOBA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/24 na atasoma tahasusi ya **PCB**

Shule ya Sekondari BUKOBA ipo umbali wa Kilometa 0.5 Kutoka stendi kuu ya mabasi . Usafiri wa taxi kutoka katika kituo cha mabasi BUKOBA MJINI unapatikana kwa nauli ya Shilingi 2000. Kwa pikipiki nauli ni Shilingi 1,000 na kwa bajaji ni 1,500.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13/8/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/8/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/8/2023**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 nyeusi zenye urefu unaozidi kwenye magoti.(picha/mshono vimeambatishwa)
ii. Mashati 2 meupe ya mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe kitambaa cha tetron ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni truck suit ya dark blue (aina ya adidas), na Bukta ya dark blue.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
*vii.* Sweta 1 ya Dark blue yenye michirizi miwili ya njano kiunoni, kwenye mikono na shingoni. (*picha yake imeambatishwa)*
viii. Nguo za kushindia: gauni (*shamba dress*) 2 za zambarau. (*mchoro/ mshono vimeambatishwa*) hijabu nayo iwe ya zambarau;
ix. Tai 1 yenye rangi ya pundamilia (*picha yake imeambatishwa)*
x. Tisheti (T-shirt) 1 ya dark blue yenye color (*picha yake imeambatishwa*)

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 14 counterbook 4Quire.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo (*orodha imeambatishwa*);
iv. Dissecting Kit
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro la 2.5’ x 6’. Yapo magodoro ya kukodishwa shuleni kwa gharama ya **Shilingi 10,000.00** kwa mwaka kwa watakaowahi;
vii. Mashuka Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*ya rangi ya Blue Bahari);*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Akaunti ya malipo ni NMB -31801100123**

**Jina la akaunti: SHULE YA SEKONDARI BUKOBA.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**AHADI YAKO**:

Nimezisoma Sheria/Kanuni hizi na kuzielewa, nitazitimiza/sitazitimiza.

Jina la Mwanafunzi…………………………………………………………………………….

Saini ya Mwanafunzi……………………………. Tarehe………………………………..

Jina la Mzazi/Mlezi:…………………………………………………………………………….

Saini ya Mzazi/Mlezi:………………………. (Mtoto atazitimiza) Tarehe………………….

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**..................................................**

**RAYMUND M. MUTAKYAHWA**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0754 076 905**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0765 051 660**
- **Mwandamizi Taaluma 0752 354 096**
- **Mwandamizi Malezi 0717 953 399**

12

**FOMU IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI**

**SHULE YA SEKONDARI BUKOBA**

**S. L. P 52,**

**BUKOBA.**

Tarehe ………………………………………

**MAHUSIANO NA MALEZI (MM)**

1. Wazazi/Walezi wanajulishwa kuwa barua yenye kuleta ujumbe muhimu kwa Mwanafunzi kama kumwombea ruhusa aje nyumbani kwa shughuli muhimu/maalum ni lazima iandikwe na Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni.

2. Kuhusu masuala mbalimbali yanayomhusu mwanafunzi, shule haitakuwa tayari kuyajadili na mtu/ndugu yeyote anayejitokeza. Bali masuala yote yamhusuyo mwanafunzi yatajadiliwa na mawasiliano yatafanyika kati ya shule na Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni. Wengine hawatakubalika, labda idhini maalum itakayoandikwa na Mzazi/Mlezi mwenyewe:

**(WAHUSIKA NI HAWA TU PEKEE NA ZIBANDIKWE PICHA ZAO pp size)**

1. JINA LA BABA: …………………………………………………… (Hai/Marehemu)

   KAZI (KAMA HAI) ……………………………………………………

   ANUANI/NAMBA YA SIMU …………………………………………………………..

2. JINA LA MAMA: …………………………………………………… (Hai/Marehemu)

   KAZI (KAMA YU HAI)…………………………………………………..

   ANUANI/ NAMBA YA SIMU ………………………………………………………..

***** Mlezi ni yule mtu uliyemteua kukuwakilisha katika masuala ya mwanafunzi huyu kama haupo.***

3. JINA LA MLEZI: ……………………………………………. …………………………….

   KAZI YAKE:…………………………………………………………………

   ANUANI /NAMBA YA SIMU…………………………………………………………………

   SAINI YA MZAZI/MLEZI: ……………………… TAREHE: …………………………………..

***NB:** ***(JAZA SEHEMU ZOTE TATU KWA WATU WATATU TOFAUTI)***

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**(Ijazwe kwa herufi kubwa)**

1. Jina kamili la Mwanafunzi ……………………………………………………………………………
2. Jinsi:……………………………………………..
3. Dini/Madhehebu ……………………………………………………………………………..
4. Tarehe ya kuzaliwa: ……………………………………………………………………………..
5. Uraia ………………………………………………………………….
6. Jina la Shule ya Msingi alikosomea …………………………………………………………….

Wilaya……………………………. Mkoa…………………………………………

Mwaka aliofanya Mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi ……………………………………

7. Jina la Mama Mzazi …………………………………………………………………………

Anwani ya mama: Wilaya ……………………… Kata …………………….. Mkoa …………………

Anaishi/haishi (futa isiyotakiwa)/ Simu…………………………………….

8. Jina kamili la Baba ………………………………………………………………………….

Anwani,Wilaya ……………………… Kata …………………….. Mkoa ………………… Anaishi/haishi (futa isiyotakiwa). Simu…………………………………….

9. Jina kamili la Mlezi ………………………………………………………………………….

Anwani, Wilaya …………………… … Kata …………………….. Mkoa …………………

10. Idadi ya watoto katika familia …………………. Kaka ……. Dada ……………………….
11. (i) Anayekulipia Ada na mahitaji mengine……………………………………………………..

    (ii) Uhusiano kati yako na jamaa anayekugharimia elimu ………………………………………
12. (i)Mwanafunzi anaishi sehemu gani ………………………………………………………..

    (ii) Anapanga/anaishi na Wazazi ……………………………………………………………….

    Kama anaishi na Ndugu, taja jina, uhusiano na anakoishi

    ………………………………...........……SIMU……........………………

    Ninakiri kuwa taarifa zote zilizojazwa hapo juu ni za kweli na ikigundulika kuwa si za kweli nichukuliwe hatua na vyombo husika.

    JINA LA MWANAFUNZI ..............…… SAINI …........……. TAREHE ……….....

    JINA LA MZAZI/MLEZI ………………SAINI ………………… TAREHE .............…

*__*NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI WA KARIBU ZAIDI*__ ………………………………

# MEDICAL EXAMINATION FORM

1. STUDENT'S NAME ………………………………………………………………………………………….
2. AGE ………………………… HEIGHT (CM) ………………….. WEIGHT (KG) ……………………………
3. BLOOD EXAMINATION: HAEMOGLOBIN ………………………………………………………………

   BLOOD GROUP ……………………………………………………………..
4. ANY ABNORMALITIES NOTED: ……………………………………………………………………….
5. STOOL EXAMINATION: ………………………………………………………………………………..
6. URINALYSIS: ……………………………………………………………………………………………
7. T.B TEST (If negative, was immunization given): ………………………………………………………….
8. EYES: ……………………………………………………………………………………………………….
9. CHEST: ……………………………………………………………………………………………………….
10. ANY CHRONIC COMPLAINTS NOT NOTED ABOVE: e.g.
    (a) ASTIMA: ……………………………………………………………………………………….
    (b) HEADACHE: ……………………………………………………………………………………..
    (c) INABILITY TO EAT CERTAIN FOOD: ………………………………………………………………...
    (d) SKIN DISEASES (and etc): ……………………………………………………………………..
11. ALSO ANYTHING ELSE THAT THE SCHOOL HEALTH STAFF SHOULD TAKE NOTE OF

………………………………………………………………………………………………………………

12. ANY TREATMENT GIVEN OR RECOMMENDED:

……………………………………………………………………………………………

**<u>NOTES</u>: If any of examinations requested above cannot be carried out. It is useful if it is noted that They have not been taken rather than writing NAD down, in case of Bilharzias/TB it is recommended that students attend the Bilharzias/TB Clinic before the come to school.**

13. **DATE**: ……………S**IGNATURE OF EXAMINER**

**DESIGNATION** ………………………………………………….

## 8. ORODHA YA VITABU


**PHYSICS**

1. Mehta V.K & Mehta R.(2008) *Principals of Physics Class Xi*; S. Chand & Company PVT. Ltd New Delh India
2. Mehta V.K & Mehta R.(2008) *Principals of Physics Class Xii*; S. Chand & Company PVT. Ltd New Delh India
3. Nelkon M. & Parker R (2004) *Advanced Level Physics 7th Ed*; Heinamann Educational Books. London
4. TIE (2020) *Advanced Level Physics Form five*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
5. TIE (2020) *Advanced Level Physics Form Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam


**CHEMISTRY**

1. Jain S.K (2008) *Conceptual Chemistry Class Xi*; S. Chan & Company PVTLtd New Delh India
2. Jain S.K (2008) *Conceptual Chemistry Class Xii*; S. Chan & Company PVTLtd New Delh India
3. TIE (2020) *Advanced Level General Cemistry Form five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
4. TIE (2020) *Advanced Level Physical Chemistry Form Five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
5. TIE (2020) *Advanced Level Organic Chemistry Form five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
6. TIE (2020) *Advanced Level Inorganic Chemistry Form Five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam

**BIOLOGY**

1. Tylor D.J etal (1997) *Biological Science 3rd Ed*; Amazon Publishers, New York
2. TIE (2020) *Advanced Level Biology Form five*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
3. TIE (2020) *Advanced Level Biology Form Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
4. Toole G. & Toole S. (2014) New Understanding Biology 4th Ed: Oxiford University Press. London United kingdom

# 9.SAMPULI ZA SARE YA SHULE

| | |
|---|---|
| **SHAMBA DRESS**  | **TIE**  |
| **T-SHIRT**  |  **SWEATER** |

| | |
|---|---|
| | |
| **SKIRT**<br> | |